SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 25 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) MACHI 2023

# TSC YASHAURIWA KUELIMISHA WALIMU KUZUIA UKATILI NA UNYANYASAJI WA WATOTO



*Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego akitoa hotuba ya kufungua Kikao Kazi cha wadau wa elimu kutoka Wilaya za Iringa na Mafinga Februari 21, 2023 mjini Iringa. Kikao Kazi hicho Kimeandaliwa na TSC kwa kushirikiana na Shirika la World Vision Tanzania.*



*Mwalimu Mkuu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu, Romuli Rojas akitoa neno la kumkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Iringa (hayupo pichani) kwa niaba ya Katibu wa TSC wakati wa kufungua Kikao Kazi cha wadau wa elimu kutoka Wilaya za Iringa na Mafinga Februari 21, 2023 mjini Iringa.*



*Mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, Zacharia Shigukulu akitoa neno kuhusu shirika hilo wakati wa kufungua Kikao Kazi cha wadau wa elimu kutoka Wilaya za Iringa na Mafinga Februari 21, 2023 mjini Iringa.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# HONGERA TSC, WORLD VISION KWA KUENDESHA MAFUNZO KUPINGA UKATILI DHIDI YA WATOTO

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la World Vision Tanzania wameanza zoezi la kuendesha mafunzo juu ya masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya walimu na kumlinda mtoto dhidi ya unyanyasaji na ukatili.

Mafunzo hayo yamewaandaa wakufunzi watakaotoa elimu hiyo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika ngazi ya shule ili watimize wajibu wao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Maadili ya kazi ya Ualimu huku wakimlinda mtoto dhidi ya ukatili na unyanyasaji unaofanyika shuleni na nje ya shule.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha Watumishi wa TSC ngazi ya wilaya, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Nidhamu za TSC ngazi ya Wilaya, Wathibiti Ubora na Maafisa Ustawi wa Jamii. Hadi kufikia Machi 1, 2023 baadhi ya Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Simiyu na Iringa zimefikiwa.

Wadau wanaohusika katika mafunzo haya wanashughulika na mtoto kwa namna moja au nyingine hivyo ni muhimu kuunganisha nguvu katika mapambano dhidi ya unyanyasaji na ukatili ambao unaendela kushamiri katika jamii zetu.

Hivyo, tunaipongeza TSC kwa kuwa na maono ya kuongeza ufahamu kwa walimu ili waweze kuwakuza watoto katika maadili mema yanayofaa na kuwasimamia kuhakikisha wanatimiza ndoto zao bila kukwamishwa na kitu chochote.

Vilevile, tunalipongeza Shirika la World Vison Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuunganisha nguvu na TSC katika kumsaidia mtoto kuwa katika mazingira salama wakati wote.

Wito wetu ni kuwasihi wadau mbalimbali kujitokeza kuongeza nguvu katika kuwezesha mafunzo haya kufanyika nchi nzima ili kuhakikisha tunaendelea kujenga Taifa la raia wema, waadilifu, wazalendo na wanaozingatia miiko na maadili ya utamaduni wetu.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama

**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***
Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania    tumeyautumishiwawalimutanzania

# TSC YASHAURIWA KUELIMISHA WALIMU KUZUIA UKATILI NA UNYANYASAJI WA WATOTO

**Na mwandishi Wetu – Iringa.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshauriwa kuongeza kasi katika kutoa elimu kwa walimu na wadau mbalimbali wa elimu ili kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji vikiwemo ubakaji, ulawiti, ushoga, vipigo na mauaji ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakiwa shuleni na nje ya shule.

Kauli hiyo imetolewa Februari 21, 2023 na Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendegu wakati akifungua kikao kazi cha siku tatu cha wadau wa elimu kutoka Wilaya za Iringa na Mufindi ambacho kimeandaliwa na TSC kwa ufadhili wa Shirika lisilo la Kiserikali la World Vision Tanzania kinachofanyika mjini Iringa.

Mkuu huyo wa Mkoa ameeleza kuwa ni muhimu kwa walimu kukumbushwa juu ya miiko na maadili ya kazi yao kwa kuwa vipo vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto vinavyofanywa na wanajamii wakiwemo baadhi ya walimu huku akisisitiza kuwa vitendo hivyo sio kwamba vinarudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa watoto tu bali vinatishia ustawi na usalama wao.

Amefafanua kuwa takwimu za hivi karibuni za matukio ya unyanyasaji dhidi ya watoto, wanawake na wanaume zinaonesha kuwa katika Mkoa wa Iringa vitendo hivyo bado vipo na vinaendelea kufanyika kwa kiwango kikubwa na hivyo ni muhimu kuongeza kasi ya kuelimisha wadau wote ili jamii iishi kwa kuzingatia maadili yanayomwandaa mtoto kuwa raia mwadilifu na mwenye tija kwa taifa.

"Mkoa wetu sio kisiwa, upo kama mikoa mingine na suala la unyanyasaji bado lipo. Tukiangalia takwimu za hivi





*Washiriki wa Kikao Kazi cha wadau wa elimu kutoka Wilaya ya Iringa na Mafinga wakisikiliza hotuba ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho uliofanyika Februari 21, 2023 mjini Iringa.*

# TSC YASHAURIWA KUELIMISHA WALIMU KUZUIA UKATILI NA UNYANYASAJI WA WATOTO



*Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa Elimu kutoka Wilaya ya Mafinga wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho uliofanyika Februari 21, 2023 mjini Iringa. Pichani wapili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mwalimu Mkuu kutoka TSC Makao Makuu, Romuli Rojas na wapili kutoka kulia ni mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, Zacharia Shigukulu.*

ya elimu ambapo katika kipindi cha miezi sita (6) iliyopita Mkoa huo umepokea shilingi zaidi ya bilioni 5.5 kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo, shilingi zaidi ya bilioni 2.9 zimetumika kulipa madeni ya watumishi wengi wao wakiwa ni walimu huku shilingi zaidi ya bilioni 8 zikitumika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo kujenga vyumba vya madarasa, maabara na matundu ya vyoo.

"Jitihada hizi zinazofanywa na Mhe. Rais wetu hazitakuwa na maana endapo hatutaongeza jitihada za kusaidia watoto wetu wasiangamie kutokana na vitendo vya mmomonyoko wa maadali vinavyozidi kuongezeka. Hivyo, pamoja na kazi kubwa na nzuri mnayoifanya TSC, ninawashauri kuongeza jitihada kuwafikia walimu na wadau wengine kuwapa elimu na mbinu za kuwalinda watoto wetu," amesema.

Hata hivyo, kiongozi huyo karibuni tuna matukio zaidi ya 2,600 ya unyanyasaji dhidi ya watoto, matukio zaidi ya 2,400 ya unyanyasaji dhidi ya wanawake na kwa upande wa wanaume tuna matukio zaidi ya 154. Ukiyajumuisha haya yote mengine yamesababisha vifo, msongo wa mawazo au maumivu yasiyoweza kutibika. Mbaya zaidi ni pale unapokuta mwalimu aliyepewa dhamana ya kuwalea watoto katika maadili mema, naye ni miongoni mwa wale wanaotenda haya," amesema Mhe. Dendego.

Amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa katika kuboresha sekta



*Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa elimu kutoka Wilaya ya Iringa wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho uliofanyika Februari 21, 2023 mjini Iringa. Pichani wapili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mwalimu Mkuu kutoka TSC Makao Makuu, Romuli Rojas na wapili kutoka kulia ni mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, Zacharia Shigukulu.*

# TSC YASHAURIWA KUELIMISHA WALIMU KUZUIA UKATILI NA UNYANYASAJI WA WATOTO

ameipongeza TSC kwa hatua inayoendelea kuchukua katika kuwafikia walimu kupitia kuandaa maadiko mbalimbali ya miradi kwa wadau wa maendeleo na kupata fedha za kutekeleza majukumu hayo huku akisema kuwa huo ndio mfano mzuri wa kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika jitihada zake za kuboresha elimu nchini.

"Ninaipongeza Menejienti ya TSC kwa ubunifu mlioutumia kwa kuandika andiko la mradi na kulipeleka na matunda yake ni haya tunayoyaona sasa kwamba World Vision Tanzania wamejitokeza kuwawezesha kifedha ili mfanye mafunzo haya muhimu. Ninawapongeza sana kwa kuona fursa hiyo na kuitumia, maeneo mengine unakuta watendaji wamekaa tu kusubiri fedha ya serikali ambazo hazitoshelezi kukidhi mahitaji yote," amesema.

Aidha, Dendego amelipongeza shirika la World Vision Tanzania kutokana na jitihada zake za kushirikiana na Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuimarisha ustawi wa watoto kwa kupambana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili, kuimarisha usawa wa kijinsia pamoja na kuboresha uchumi wa wananchi katika maeneo mbalimbali.

"Ninawashukuru World Vision Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na Serikali kutekeleza shughuli mbalimbali zenye lengo la kukuza usawa wa kijinsia na kupinga kila aina ya ukatili na uonevu dhidi ya watoto. Ninaelewa kuwa, moja ya njia ya kukuza usawa huo wa kijinsia ni kuboresha mazingira ya kusomea na kujifunzia, ikiwa ni pamoja na kuongeza vyumba vya madarasa na madawati pamoja na kununua vitabu kwa ajili ya shule ili kuhakikisha watoto wa jinsia zote wanapata fursa ya kuendelezwa," amesema.

Akitoa neno la utangulizi kwa niaba ya Katibu wa TSC, Mwalimu Mkuu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu, Romuli Rojas amesema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 TSC iliandaa andiko mradi linaloitwa 'Enhansing Teachers' Ethics and Professional Conduct in Primary and Secondary Schools' (ETEP) ikiwa ni moja ya juhudi za kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili kupata rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuimarisha maadili ya walimu ili watoe huduma bora kwa wanafunzi.

Ameongeza kuwa Kikao Kazi hicho kinawahusisha washiriki 20 ambao ni Maofisa wa TSC, Wajumbe wa Kamati za Wilaya, Wadhibiti Ubora wa Shule, Maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya pamoja na Maafisa elimu wa Wilaya wote kutoka Wilaya za Iringa na Mufindi na kusema kuwa watakuwa wawezeshaji kwenye ngazi ya shule kwa utaratibu ambao wilaya husika itaupanga




*Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wakufunzi wa mafunzo (waliosimama) wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho uliofanyika Februari 21, 2023 mjini Iringa. Pichani, wapili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mwalimu Mkuu kutoka TSC Makao Makuu, Romuli Rojas na wapili kutoka kulia ni Mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, Zacharia Shigukulu.*

# TSC YASHAURIWA KUELIMISHA WALIMU KUZUIA UKATILI NA UNYANYASAJI WA WATOTO

kwa kushirikiana na Shirika la World Vision Tanzania ili kufikisha elimu kwa walimu ngazi ya Shule na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata.

Kwa upande wa mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, Zacharia Shigukulu amesema Shirika hilo limeingia makubaliano na Serikali ya namna ya kushiriki kwa pamoja katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa watoto ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wadau ili kupiga vita vitendo hivyo kwa watoto na wanawake.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa World Vision Tanzania itaendelea kufanya kazi kwa pamoja na Serikali katika kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili kwa watoto. Huku kwetu Iringa vipo viashiria vingi vinavyoonesha kwamba wapo watu wanaojihusisha na vitendo hivyo. Lakini kwa bahati mbaya zaidi vimekwenda mpaka vimegusa walimu wetu ambao wanajukumu la kuwalea watoto," amesema Zacharia.

Ameongeza kuwa, "kupitia mafunzo haya tuna amini kuwa elimu itakayotolewa itawafikia walengwa ili kupunguza na hatimaye kutokomeza vitendo hivi. Tunataka Taifa liendelee kwa kuwa na watoto wenye maadili mema, waliofundishwa vizuri na ambao hawajaathirika kisaikolojia ili tuwakuze vizuri na watakapokuwa watu wazima wakatekeleze majukumu yao vizuri kwa ajili ya kuleta maendeleo katika Taifa letu la Tanzania."





*Mafunzo yakiendelea kutolewa wakati wa Kikao Kazi cha wadau wa elimu kutoka Wilaya ya Iringa na Mafinga kinachofanyika Februari 21 – 23, 2023 mjini Iringa.*

**OFISI YA RAIS**
**TUME YA UTUMISHI**
**WA WALIMU (TSC)**

# Shukrani

Tume, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunatoa shukrani zetu kwa **Mhe. David Silinde, Prof. Riziki S. Shemdoe, Dkt. Grace E. Magembe, Bw. Ramadhani Kailima** kwa kipindi chote mlichotumikia Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**Pia tunawapongeza kwa kuteuliwa katika nafasi zenu mpya na tunawatakia kila la kheri.**

#Kazi Iendelee



www.tsc.go.tz   secretary@tsc.go.tz   Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# NHIF YAIKABIDHI TUME MAJINA YA WALIMU WALIOFANYA UBADHIRIFU



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika kikao kilichoikutanisha Menejimenti ya TSC na ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kilichofanyika Februari 27, 2023 katika ofisi za NHIF Makao Makuu jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu Dodoma**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umekabidhi kwa Tume ya Utumishi ya Walimu jumla ya majina 78 ya Walimu waliobainika kughushi nyaraka mbalimbali za wategemezi wao pamoja na matumizi mabaya ya kadi za matibabu.

Walimu hao wamehusika kwa nyakati mbalimbali kughushi nyaraka za vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya ndoa kwa lengo la kutaka kuthibitisha uhusiano wao na wahusika hao ili waweze kusajiliwa na Mfuko.

Makabidhiano hayo ya majina yamefanyika Februari 27, 2023 Makao Makuu ya NHIF Jijini Dodoma wakati wa kikao kati ya Menejimenti ya Mfuko na ya Tume ya Utumishi wa Walimu. Katika kikao hicho ilitolewa ripoti inayoonesha namna Walimu hao walivyohusika katika vitendo vya udanganyifu pamoja na hasara waliyoisababisha kwa Mfuko.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi wa NHIF, Bw. Bernard Konga alisema Mfuko umeshachukua hatua mbalimbali kwa watuhumiwa hao ambao walikiri kutenda makosa hayo. ikiwemo kuwafungulia kesi, kuwafungia matumizi ya kadi na kuwataka kurejesha fedha ambazo zilitumika kuhudumia wategemezi wasio halali.

"Tunachukua hatua



*Mkurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bw. Bernard Konga akiongoza kikao kilichoikutanisha Menejimenti ya TSC na ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kilichofanyika Februari 27, 2023 katika ofisi za NHIF Makao Makuu jijini Dodoma.*

# NHIF YAIKABIDHI TUME MAJINA YA WALIMU WALIOFANYA UBADHIRIFU

nyingi kwa watuhumiwa wa udanganyifu na mpaka sasa kuna kesi zinaendelea katika Mikoa ya Geita, Dodoma na Dar es Salaam, kadi za matibabu za watuhumiwa hao zimefungiwa pamoja na kuwaandikia barua za onyo hivyo tunaomba tushirikiane katika hili ili kukomesha vitendo hivi ambavyo vina madhara makubwa kwa Mfuko," alisema Bw. Konga.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwalimu Paulina Nkwama alisema kuwa vitendo vilivyofanywa na Walimu hao haviwezi kukubalika kwa kuwa ni ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma hivyo kupitia mamlaka ya tume hiyo hatua zitachukuliwa.

Aidha alikubali Tume hiyo kushirikiana na Mfuko kwa karibu katika kupambana na wimbi hilo la udanganyifu unaofanywa na walimu pamoja na kuelimisha



*Picha ya pamoja kati ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC na ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mara baada ya kumalizika kwa kikao kilichofanyika Februari 27, 2023 katika ofisi za NHIF Makao Makuu jijini Dodoma.*

madhara ya kughushi au kufanya udanganyifu wowote kupitia kadi ya matibabu.

Awali akiwasilisha taarifa ya uchunguzi wa udanganyifu uliofanywa na Watumishi wa Umma, Meneja wa Kitengo cha Kupambana na Udanganyifu cha NHIF Dkt. Rose Ntundu alisema kuwa kati ya Watumishi wa Umma 99 waliobainika kufanya udanganyifu, 78 ni Walimu wa Shule za Serikali za Msingi na Sekondari.

"Udanganyifu ambao wamekuwa wakiufanya ni pamoja na kughushi nyaraka kwa lengo la kutaka kuthibisha kuwa ni wategemezi wao lakini pia kutumia vibaya kadi zao kwa kuchukua dawa katika hospitali mbalimbali kwa kutumia kadi zao na kula njama na baadhi ya vituo vya matibabu kwa kusaini fomu za matibabu na wao kupewa fedha kidogo na vituo hivyo kuwasilisha madai kubwa kwa Mfuko,"

Mfuko umejipanga kupambana na udanganyifu kwa kushirikiana na vyombo vya sheria, kuimarisha mifumo kwa kutumia TEHAMA yake kwa lengo la kudhibiti udanganyifu na hivi karibuni Mfuko utaanza matumizi ya mfumo wa kuwatambua wanachama wake kupitia sura zao au alama za vidole wanapokwenda kupata huduma.



*Kikao kati ya Menejimenti ya TSC na ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kilichofanyika Februari 27, 2023 katika ofisi za NHIF Makao Makuu jijini Dodoma kikiwa kinaendelea.*




# MWANACHAMA WA NHIF

- **Usisaini fomu** ya matibabu ya NHIF **kabla** ya kumaliza huduma katika kituo cha huduma.
- **Hakiki huduma** zilizojazwa kama **ndizo ulizopata** na zimejazwa **gharama zake** na **fomu imefungwa** kwa mstari maeneo yasiyojazwa huduma **ndipo usaini.**
- **Nakala ya fomu** ya matibabu baada ya kupata huduma **ni haki yako**. Ondoka na nakala yako.
- **Ondoka na kitambulisho** chako cha NHIF baada ya huduma.
- **Usitoe kadi yako** ya NHIF kwa matumizi ya **matibabu ya mtu mwingine**. Ni kosa kisheria.

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**Piga 199 bure huduma kwa wateja**

**Piga 0800 111163 kutoa taarifa za siri za udanganyifu**

Uhakika wa Matibabu kwa Wote

nhiftz www.nhif.or.tz NHIF Online Tv

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

# PONGEZI

Tume, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

## Tunakuahidi Ushirikiano

#Kazi Iendelee



Mhe. Deogratius J. Ndejembi

www.tsc.go.tz secretary@tsc.go.tz Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# MAKATIBU TAWALA WA MIKOA WATAKIWA KUFANYA MSAWAZO WA WALIMU

- *Ni kutoka shule zenye ziada na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi;*
- *Upungufu huo hutokana na kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kufariki; na*
- *Ajira na msawazo vitasaidia kuendana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa shule.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. David Silinde (Mb), amesema Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara kufanya msawazo wa Walimu kutoka shule zenye ziada na kuwapeleka katika shule zenye upungufu zaidi.

Alisema hayo hivi karibuni Bungeni Jijini Dodoma wakati akijibu Swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Martha Mariki, aliyetaka kujua kuna mpango gani wa kutatua changamoto ya uhaba wa Walimu katika shule za pembezoni.

Mhe. Silinde alisema Serikali imekuwa ikitoa ajira ili kukabiliana na upungufu wa Walimu shuleni, upungufu unaotokana na Walimu kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa, kufariki na kuendana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa shule.

Alisema tangu mwaka 2018/19 hadi mwaka 2021/22, Serikali imeajiri jumla ya Walimu 26,598 wakiwemo 16,640 wa Shule za Msingi na 9,958 wa Shule za Sekondari.



Aidha, Mhe. Silinde alisema Serikali inahakikisha Walimu wanaajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika shule zenye uhitaji zaidi, hususan zilizoko maeneo ya vijijini na pembezoni.

Alisema Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliboresha Mfumo Maalum wa Maombi ya Ajira na Upangaji wa Walimu ujulikanao kama 'Teachers Allocation Protocol (TAP)', kupitia mfumo huo shule zenye upungufu mkubwa wa Walimu hususan zilizoko vijijini na maeneo ya pembezoni hubainishwa.

Mhe. Silinde alisema kuwa Serikali itaendelea kuajiri Walimu kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha ili kukabiliana na uhaba wa Walimu hususani katika maeneo ya pembezoni na vijijini.

# CHUO KIKUU CHA AGA KHAN CHATAMBUA MCHANGO WA TSC KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI



*Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia) katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara na Taasisi zinazosimamia Elimu katika nchi za Afirika Mashariki baada ya kupokea tuzo kutoka kwa uongozi wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan ya kutambua mchango wa Tume katika sekta ya elimu nchini, wakati wa mkutano uliofanjika tarehe 01-03/02/2023 Jijini Dar es Salaam. Pichani, wa tano kutoka kulia ni Profesa Jane Rarieye (Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan).*

**Na Mwandishi wetu - Dar es Salaam.**

Chuo Kikuu cha Aga Khan kupitia Taasisi yake ya Maendeleo ya Elimu, Afrika Mashariki imetambua mchango wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika sekta ya Elimu nchini, ambapo Katibu wa Tume ya Utumishi wa walimu Mwl. Paulina Nkwama na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu TSC Bw. Zachary Dida ni miongoni mwa wadau wa elimu walioalikwa kuhudhuria mkutano wa kimataifa kuhusu Elimu uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Aga Khan Jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo ulifanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 01-03/2023 huku ukiwakutanisha wadau mbalimbali wa Elimu kutoka nchi za Afika Mashariki za Tanzania, Kenya na Uganda na ulikuwa na lengo la kujadili ujenzi wa mifumo himilivu ya elimu wakati wa majanga.

Kwa upande wa Tanzania, Tume ya Utumishi wa Walimu, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa Wizara na Taasisi za Serikali zilizoalikwa katika mkutano huo.

Wakizungumza katika mkutano huo, wadau wa Elimu wa nchi za Afrika Mashariki wamekubaliana katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ya Elimu ili kukabiliana na majanga yanayojitokeza ambayo yanaathiri mchakato wa



*Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia walioko mbele) katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara na Taasisi zinazosimamia Elimu katika nchi za Afirika Mashariki wakati wa mkutano wa kimataifa kuhuhu elimu uliofanyika katika Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan mnamo tarehe 01-03/02/2023 Jijini Dar es Salaam. Wa pili kutoka kushoto walioko mbele ni Profesa Jane Rarieye (Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan).*

# CHUO KIKUU CHA AGA KHAN CHATAMBUA MCHANGO WA TSC KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI

ufundishaji na ujifunzaji.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi kutoka Wizara na Taasisi za Serikali zilizoalikwa katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya alieleza kuwa Serikali ya Tanzania inaamini matumizi ya TEHAMA katika Sekta ya Elimu ni ya lazima, na kwamba Serikali imewapatia Vishikwambi walimu wote nchini wanaofundisha Shule za Msingi na Sekondari pamoja na wakufunzi wa vyuo vya Ualimu.

Aliongeza kuwa kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania vitabu vyote vya kiada kwa shule za Msingi na Sekondari vinapatikana mtandaoni hivyo walimu na wanafunzi wakati wowote wanaweza kuvisoma na kujifunza.

Vilevile alisema kuwa kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kuna studio inayorekodi vipindi kwa ajili ya ufundishaji, vipindi ambavyo vilitumika na kusaidia sana suala la ufundishaji na ujifunzaji wakati wa janga la UVIKO-19.

Pia alisema kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Tume ya Utumishi wa walimu kwa sasa inaendesha mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo walimu katika utekelezaji wa majukumu yao na uzingatiaji wa maadili ya kazi ya ualimu.

Naye Profesa Jane Rarieye ambaye ni Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan alisema katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji nchi za Afrika Mashariki hazina budi kuwekeza kwa walimu na wanafunzi katika matumizi ya TEHAMA.



*Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia walioketi) katika picha ya pamoja na wanafunzi wa kitanzania wanaosoma katika Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan wakati wa mkutano wa kimataifa kuhusu elimu uliofanyika chuoni hapo mnamo tarehe 01-03/02/2023. Aliyesimama nyuma ya Katibu ni Bw. Mlekwa M. Nuhu mtumishi wa TSC ambaye kwa sasa anasoma katika chuo hicho, na wa pili kutoka kulia waliosimama nyuma ni Bw. Zachary Dida Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu TSC.*

# CHUO KIKUU CHA AGA KHAN CHATAMBUA MCHANGO WA TSC KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI



*Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia walioketi), Bw. Zachary Dida Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu TSC (aliyesimama nyuma katikati) na viongozi wa Wizara na Taasisi zinazosimamia Elimu Tanzania katika picha ya pamoja na uongozi wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan wakati wa mkutano wa kimataifa kuhusu elimu uliofanyika tarehe 01-03/02/2023 Jijini Dar es Salaam. Wa tatu kutoka kushoto walioketi ni Profesa Jane Rarieye (Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan).*

"Katika kufundisha wanafunzi tunahitaji kuangalia matumizi ya TEHAMA ili kukabiliana na majanga yanayoweza kuathiri ujifunzaji. Sote tunakumbuka namna ambavyo mifumo yetu ya elimu ilivyotikisika wakati wa janga la UVIKO-19 lililoikumba Dunia na kupelekea mambo kuharibika, hivyo tuna kila sababu ya kujenga mifumo himilivu ya elimu katika siku zijazo. Matumizi ya TEHAMA ndiyo nyenzo pekee katika kukabiliana na majanga kama hayo," alisema Profesa Jane Rarieye.

Katika kutambua mchango wa wadau wa elimu nchini, chuo Kikuu cha Aga Khan kilitoa tuzo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wakati wa ufungaji wa mkutano huo.

Akiongea na waandishi wa habari baada ya mkutano huo, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama aliushukuru uongozi wa Taasisi ya Maendeleo ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Aga Khan kwa kuendesha mkutano huo wa Kimataifa kuhusu elimu pamoja na tuzo ambayo Taasisi hiyo imeitoa kwa Tume hiyo kwamba ni heshima kubwa ambayo Taasisi hiyo imeipa TSC na kusema kuwa huo ni mwanzo mzuri wa ushirikiano.

"Naushukuru sana uongozi wa Chuo Kikuu cha Aga Khan kwa kutambua mchango wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika sekta ya elimu nchini kwa kutupatia tuzo hii. Hii ni heshima kubwa ambayo wametupatia. Tunaamini huu ni mwanzo mzuri wa ushirikiano baina Tume na Chuo Kikuu cha Aga Khan," alisema Mwl. Paulina Nkwama.

# MANISPAA YA SHINYANGA YAENDESHA MAFUNZO YA MATUMIZI SAHIHI YA VISHIKWAMBI KWA WALIMU

- *Manispaa ya Shinyanga ilipata mgao wa vishikwambi 1,019;*
- *Vyote vyagawiwa kwa Walimu, Maafisa Elimu wa Kata na Viongozi wanaosimamia Sekta ya Elimu;*
- *Kuleta tija zaidi kwa Walimu katika kuandaa masomo, kufundisha, kutunga mitihani, kusahahihisha mitihani na kuandaa taarifa za utendaji kazi.*

**Na. Mwandishi Wetu – Shinyanga.**



Tarehe 13 Desemba, 2022 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (MB), aliwaelekeza Katibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kusimamia kikamilifu zoezi la ugawaji wa vishikwambi kwa Walimu wote vilivyotolewa na Serikali.

Kupitia Mpango huo, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilibahatika kupata mgao wa vishikwambi 1,019 ambavyo ilivigawa kwa Walimu wote, Maafisa Elimu wa Kata na Viongozi wote wanaosimamia Sekta ya Elimu.



Baada ya kukamilika kwa ugawaji wa vishikwambi hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Ndg. Jomaary Mrisho Satura, kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo cha Ushirika Kizumbi kilichopo Mkoani Shinyanga hivi karibuni waliendesha mafunzo ya matumizi sahihi ya vishikwambi hivyo ili kuleta tija zaidi kwa

# MANISPAA YA SHINYANGA YAENDESHA MAFUNZO YA MATUMIZI SAHIHI YA VISHIKWAMBI KWA WALIMU





kuwasaidia Walimu kuweza kuandaa Masomo, kufundisha, kutunga mitihani, kusahahihisha mitihani na kuandaa taarifa za utendaji kazi kwa haraka zaidi.

Kwa upande wake Ndg. Satura baada ya kushuhudia mafunzo hayo, aliwasisitiza Walimu kutokua na sababu yoyote ya kushindwa kushiriki kikamilifu katika jitihada za Serikali katika kuboresha kiwango cha Elimu nchini.

"Vishikwambi hivi tulivyogawiwa na Serikali yetu pendwa, vinaenda kusaidia kupunguza malalamiko kwa Walimu kwa kiwango kikubwa kwani sasa Mwalimu mmoja atakuwa na uwezo wa kufundisha shule zaidi ya moja kwani kazi ya kuandaa masomo, kufundisha, kutunga mitihani, kusahihisha na kuandaa taarifa sasa itakuwa imerahisishwa kwa kiwango kikubwa iwapo vishikwambi hivi tulivyogawiwa vitatumika kwa usahihi kama tulivyojifunza hapa." Alisema Mkurugenzi Satura

Aidha, alikubaliana na wazo la Chuo cha Ushirika Kizumbi kufanya mpango maalum wa kurekodi vipindi vya masomo kutoka kwa Walimu wenye umahili mkubwa na kisha kushirikishana kupitia vishikwambi hivyo ambapo kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa itawajibika kununua skrini za runinga na kuziweka katika vyumba maalumu kwenye kila shule ili kuwezesha ufundishwaji na ujifunzaji wanafunzi kwa masomo ambayo katika shule husika Walimu wa masomo husika hawapo.



# WADAU WA ELIMU MKOA WA LINDI WASHAURIWA KUONGEZA KASI KATIKA KUWASIMAMIA WALIMU

**Na. Mwandishi Wetu – Lindi.**

Wadau wa Elimu Mkoa wa Lindi wameshauriwa kuongeza ufanizi katika usimamizi wa shughuli za elimu na kuwasaidia walimu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na za Utumishi wa Umma.

Ushauri huo umetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili katika kikao cha maabara ya elimu Mkoa wa Lindi kilichofanyika tarehe 14 na 15 Februari, 2023 wilayani Nachingwea.

Kikao hicho kilichoandaliwa na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Lindi kililenga kufanya tathmini ya utendaji kazi wa idara ya elimu katika mkoa huo kwa mwaka 2022 na kuweka mipango ya mwaka 2023.

Mkuwili ameeleza kuwa elimu mkoa wa lindi uweze kuwa bora ni lazima kila mdau azingatie usimamizi mzuri wa utumishi wa walimu ili walimu waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi na hivyo, kuinua kiwango cha elimu.

Akiwasilisha mada yake iliyolenga umuhimu wa TSC katika kuinua ubora wa ufundishaji na ujifunzaji na ufundishaji, Muwili amesema usimamizi wa utumishi wa walimu umepitia hatua mbalimbali za mabadiliko kabla na baada ya uhuru ikiwa ni jitihada za serikali kutafuta namna bora ya kusimamia kada ya ualimu.

"Baada ya uhuru mwaka 1962 Serikali iliunda chombo cha usimamizi wa walimu chini ya sheria namba 6 ya mwaka 1962 chombo kilichojulikana kama "Unified Teaching Service" (UTS) kilichoshughulikia utumishi wa walimu wote wa serikali na wa sekta binafsi. Mwaka 1989 chini ya sheria namba 1 ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili.*

1989 iliundwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), mwaka 2002 chini ya sheria Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 baada ya kupitia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 iliundwa Tume ya Utumishi wa Umma ambapo TSC ilikuwa ni idara ya Tume hiyo ikijulikana kama Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD), Pamoja mabadiliko hayo, changamoto kadhaa zilijitokeza na kusababisha kutungwa kwa Sheria ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2016 na kuanzishwa kwa TSC ya sasa," alisema.

Alifafanua kuwa, Kifungu cha 5 (a) - (L) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 kimeipa TSC majukumu makuu katika kusimamia Utumishi wa Walimu ambayo ni pamoja na masuala ya ajira na maendeleo ya Utumishi wa Walimu na kusimamia maadili na nidhamu ya Utumishi wa Walimu.

Katika kusimamia maadili ya Utumishi wa walimu Nguzo za maadili zimeandaliwa ili kumsaidia mwalimu kutekeleza mjukumu yake kwa weledi na ufanisi, hivyo amewashauri wadao hao wa elimu kusimamia walimu ili wazingatie maadili hayo.

Akizifafanua nguzo hizo, Mkuwili amesema kuwa mwalimu katika kutekeleza majukumu yake anapaswa kuwa na mwendo na tabia njema kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, kutimiza majukumu yake kwa ufanisi, kutokuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi na kuhakikisha kuwa anawalinda wanafunzi na masuala yote yanayohusiana na mambo yasiyozingatia maadili kama vile kujihusisha na ngono.

"Mwalimu anapaswa kuzingatia wajibu katika kazi yake ya ualimu. Yaani wajibu wake kwa mtoto, wajibu kwa taaluma yake, wajibu kwa watumishi wenzake, wajibu kwa mkuu wake wa shule, Wajibu kwa mwajiri wake, wajibu kwa mzazi, wajibu kwa jamii na wajibu kwa Taifa lake,"alisema.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alimalizia kwa kusema TSC inaamini kuwa kama mwalimu atafanya kazi yake kwa kuzingatia miiko na maadili ya kazi hiyo tendo la ujifunzaji na ufundishaji litafanikiwa vizuri na kwamba kiwango cha elimu katika mkoa wa Lindi na Tanzania kwa ujumla kitaendelea kukua.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

# PONGEZI

Tume, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

## Tunakuahidi Ushirikiano

#Kazi Iendelee

**Bw. Adolf H. Ndunguru**



www.tsc.go.tz secretary@tsc.go.tz Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# TET YAANZA UANDAAJI WA MAKALA ZA PICHA JONGEFU ZA MODULI SABA ZA KIELETRONIKI





**Na. Mwandishi Wetu – Tanga na Arusha.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imeanza kazi ya kuandaa picha jongefu (video) mbalimbali za moduli saba za kieletroniki zitakazotumika katika Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kazi inayofanyika katika Mkoa wa Tanga na Arusha.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Habari na Machapisho wa TET, Ndg. Kwangu Masalu, alisema kuwa TET kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliandaa moduli 10 za Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) chini ya Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Ndg. Masalu alisema kuwa, kati ya moduli hizo 10 moduli saba zinatakiwa kutengenezwa na maudhui yake kuwa katika mfumo wa kieletroniki ili kuziboresha na hivyo kuongeza ufanisi katika ujifunzaji kwa kutumia mfumo wa ujifunzaji wa TET ambao ni Learning Management System (LMS).

Kwa upande wake Dkt. Fika Mwakabungu, Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Mitaala kutoka TET aliongeza kuwa, Idara hiyo imehakikisha kuwa Walimu wanaorekodiwa ni mahiri na hivyo anatarajia kuwa picha jongefu hizo za mfano zitaleta tija kubwa katika mafunzo ya MEWAKA kwani zimeshirikisha wataalamu mbalimbali ili kuhakikisha picha hizo jongefu zinazoandaliwa zinakuwa bora na za mfano.

Aidha, Mratibu wa Kazi hiyo Ndg. Japhet Magumbo, alisema kuwa zoezi la kuchukua picha jongefu hizo linafanyika kwa ushirikiano baina ya Wanafunzi na Walimu wa Shule za Msingi na kusema kuwa picha hizo zitasaidia kuonesha namna ambavyo Wanafunzi wakijifunza vizuri kutoka kwa Mwalimu mahiri na wanaweza kutumia maarifa hayo hata wakiwa mazingira ya nyumbani katika kutatua changamoto za kila siku.

Hata hivyo, aliongeza kuwa picha hizo zitaonesha namna Mwalimu anavyomsaidia Mwanafunzi kushirikiana na wenzake na kumjengea tabia njema mwanafunzi awapo katika mazingira ya shule na nyumbani.

Mratibu huyo alisema kuwa, kwa Mkoa wa Tanga wamefanikiwa kuchukua picha hizo katika Shule za Msingi zilizopo Halmashauri ya Korogwe na kwa Mkoa wa Arusha vipindi vitachukuliwa katika Shule za Msingi zilizopo Halmashauri ya Meru, Wilaya ya Arusha na Arusha Mjini.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

# PONGEZI

Tume, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

## Tunakuahidi Ushirikiano

#Kazi Iendelee

Bw. Sospeter Mambile Mtwale



www.tsc.go.tz secretary@tsc.go.tz Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# TSC, WORLD VISION WATOA MAFUNZO KUIMARISHA MAADILI YA WALIMU, KUMLINDA MTOTO




*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude akifungua mafunzo kuhusu Wajibu wa Mwalimu katika masuala ya Ajira, Maadili na Wajibu wa Jamii katika kumlinda Mtoto. Mafunzo hayo yamefanyika mjini Shinyanga Februari 1, 2023, yameandaliwa na TSC kwa kushirikiana na Taasisi ya World Vision Tanzania na yamehusisha wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu.*




*Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya akitoa neno la kumkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Kishapu (hayupo pichani) ili afungue mafunzo ya wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu. Mafunzo hayo yanafanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga.*

**Na Mwandishi Wetu – Shinyanga.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya World Vision Tanzania wameandaa mafunzo kwa Wadau mbalimbali wa Elimu kuhusu Wajibu wa Mwalimu katika masuala ya Ajira, Maadili na Ushughulikiaji wa Mashauri ya Nidhamu, kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya haki, ustawi wa mtoto na wajibu wa mzazi/mlezi katika kumlea na kumlinda mtoto.

Mafunzo hayo ya siku tatu, Februari 1 – 3, 2023 yaliyofanyikia mjini Shinyanga yamehusisha wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu ambapo washiriki ni Watumishi wa TSC, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Nidhamu za TSC ngazi ya Wilaya, Wathibiti Ubora na Maafisa Ustawi wa Jamii ili kuwezesha washiriki hao kutoa elimu hiyo kwa walimu katika ngazi ya shule.

Mafunzo hayo yalifunguliwa Februari 1, 2023 na Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ambapo amesema mmomonyoko wa




*Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wadau wa elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yanayofanyika Februari 1 – 3, mjini Shinyanga.*



*Kiongozi wa Elimu wa Taasisi ya World Vision Tanzania, Jennifer Mhando akitoa neno la shukrani kwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu (hayupo pichani) mara baada ya ufunguzi wa mafunzo ya wadau wa elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu Februari 1, 2023 mjini Shinyanga.*

# TSC, WORLD VISION WATOA MAFUNZO KUIMARISHA MAADILI YA WALIMU, KUMLINDA MTOTO



*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude (wa pili kutoka kulia) akikata utepe kuzindua vitini vitakavyotumika kutoa mafunzo kwa walimu katika ngazi ya shule juu ya Wajibu wa Mwalimu katika masuala ya Ajira, Maadili na Wajibu wa Jamii katika kumlinda Mtoto. Amezindua vitini hivyo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wadau wa elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu Februari 1, 2023 mjini Shinyanga.*

maadili katika jamii ni agenda ya Kitaifa inayohitaji nguvu ya pamoja ili kumlinda mtoto dhidi ya ukatili unaotokea mara kwa mara katika jamii.

Kiongozi huyo alifafanua kuwa inasikitisha kuona wapo baadhi ya walimu wanajihusisha na vitendo vya uvunjifu wa maadili hususan kwa watoto wakati jamii imewaamini na kuwakabidhi wanafunzi ili wawalee huku akisema kuwa ukiukwaji huo unasababisha baadhi ya wazazi kuanza kukata tamaa kuwapeleka watoto shule hususan wale waliotakiwa kujiunga kidato cha kwanza kwa kuona kuwa watoto hawapati kile wanachostahili.

"Mmomonyoko wa maadili ya watu wakiwemo walimu imekuwa ni tatizo kubwa. Agenda hii tunayo kama taifa na hata katika Mkoa wetu wa Shinyanga tunatambua na tupo kwenye mikakati ya kukabiliana nayo. Tunashukuru TSC pamoja na World Vision kwa kuja na wazo hili la kuwakusanya wadau hawa ambao kila mmoja anahusika kwa mwalimu na kwa mtoto."

"Mambo haya tunayafanya sisi ambao tumekabidhiwa watoto, hatuwalei katika misingi inayotakiwa. Baadhi ya walimu hawana maadili, wanaanzisha mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, wengine wanawapa mimba wanafunzi na wengine kutoa adhabu kupitiliza nk. Wakati mwingi haya yanapotokea baadhi ya wazazi wanakata tamaa kupeleka watoto shule kwa kuwa







*Washiriki wa mafunzo ya wadau wa elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yanayofanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga wakiwa kwenye mafunzo hayo.*

# TSC, WORLD VISION WATOA MAFUNZO KUIMARISHA MAADILI YA WALIMU, KUMLINDA MTOTO

wanaona watoto hawaendi kupata kitu wanachotakiwa kupata," alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya aliongeza kuwa wapo baadhi ya walimu ambao hawatimizi wajibu wao, hawafundishi, wanakuwa na dharura mara kwa mara za kuwa nje ya kituo cha kazi huku wakipokea mishahara ambayo hawaifanyii kazi, hivyo amewataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanakwenda kuwaelimisha walimu juu ya umuhimu wa kumpatia mtoto haki yake ya kufundishwa na kulindwa dhidi ya uovu wowote.

Aliongeza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kuimarisha miundombinu ya shule ikiwemo ujenzi wa madarasa, vyoo, madawati na sasa ujenzi wa nyumba za walimu akiwa na matarajio kwamba watoto wapate elimu bora.

"Pamoja na juhudi hizi za Rais, bado unakuta mpaka leo Januari imekwisha tupo mwezi Februari lakini kuna wanafunzi wamefaulu kwenda kidato cha kwanza lakini hawajafika shuleni. Miaka michache iliyopita tulikuwa tunasema madarasa hayatoshi sasa hivi madarasa ni mengi tunatafuta watoto waje wasome. Lazima tuwaeleze walimu kuwa wana wajibu mkubwa kuwafanya watoto wapende na wafurahie kuwepo shuleni," alisema.



*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mkoa wa Simiyu wakati wa mafuzo ya washiriki hao yanayofanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga. Pichani, wa pili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya na wa pili kutoka kulia (waliokaa) ni Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura.*



*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mkoa wa Shinyanga wakati wa mafuzo ya washiriki hao yanayofanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga. Pichani, wa pili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya na wa pili kutoka kulia (waliokaa) ni Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura.*

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya alisema kumekuwa na changamoto ya walimu wanaojihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa Maadili ya Kazi ya Ualimu na hivyo kuifanya kazi ya Ualimu ipoteze hadhi yake.

"Ni jambo lililo dhahiri kuwa Mwalimu anayezingatia Maadili na Miiko ya kazi yake ana mchango mkubwa katika wa kukuza taaluma ya ualimu na kuifanya Shule iwe salama," alisema.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa pamoja na jitihada ambazo Tume hiyo inazichukuwa ikiwemo kutoa elimu kuhusu

# TSC, WORLD VISION WATOA MAFUNZO KUIMARISHA MAADILI YA WALIMU, KUMLINDA MTOTO

maadili ya kazi ya ualimu, baadhi ya walimu wamemeendela kukiuka maadili ya utumishi wao ambapo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22 jumla ya walimu 11,022 walipatikana na makosa mbalimbali na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kwa mujibu wa Muya, Makosa hayo yaliyofanyika ni pamoja na utoro, kughushi vyeti vya kitaaluma, mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, ukaidi na ulevi wakati wa kazi.

"Ni matumaini yangu kuwa kikao kazi hiki kitawawezesha washiriki wa mafunzo ya kujengeana uwezo kuyaelewa vyema Masuala ya Ajira, Wajibu wa Mwalimu na Kanuni za Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ili hatimaye wakatoe mafunzo kwa Walimu waliopo shuleni," alisema.

Naye Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura alisema Taasisi hiyo inalenga kuhakikisha



*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mkoa wa Tabora wakati wa mafuzo ya washiriki hao yanayofanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga. Pichani, wa pili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya na wa pili kutoka kulia (waliokaa) ni Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura.*

maisha ya mtoto yanakuwa mazuri na dunia inakuwa sehemu salama zaidi kwa mtoto kuishi.

Aliongeza kuwa Taasisi hiyo imeamua kushirikiana na TSC kutoa mafunzo hayo kwa kuwa Tume hiyo ndiyo inayosimamia Maadili na Nidhamu ya walimu na kwa kuwa mtoto yupo na mwalimu kwa muda mrefu zaidi ni muhimu TSC ichukue jukumu la kuwaelimisha walimu ili waishi na watoto kwa usalama.

"Kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha tabia za walimu ili waendelee kuishi na watoto wetu vizuri wanapokuwa shuleni. Shuleni ni sehemu ambapo mtoto anakaa muda mwingi zaidi kuliko nyumbani na uhalifu dhidi ya watoto unaweza kutokea shuleni zaidi kuliko hata nyumbani. Hivyo, baada ya mafunzo haya washiriki watakwenda kuwaelimisha walimu ambao ndio walengwa. Tunaamini kwa kufanya hivyo vitendo vya uhalifu dhidi ya watoto vitapungua," alisema Jacline.



*Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mhe. Joseph Mkude (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC pamoja na watumishi wa Taasisi ya World Vision Tanzania walioshiriki mafunzo ya wadau wa elimu kutoka Wilaya Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yanayofanyika Februari 1 – 3, 2023 mjini Shinyanga. Pichani, wa pili kutoka kushoto (waliokaa) ni Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Fatuma Muya na wa pili kutoka kulia (waliokaa) ni Meneja Mradi wa Taasisi ya World Vision Tanzania Kanda ya Nzega, Jackine Kaihura.*

# TET YAENDESHA MAFUNZO YA MTAALA NA MBINU ZA UFUNDISHAJI KIBITI – PWANI

- *Walimu 280 wa Shule za Sekondari zilizopo katika Wilaya ya Kibiti kunufaika;*
- *Walimu wa masomo ya Sanaa, Lugha, Sayansi, Hisabati, Kilimo na Biashara wakihusika.*

**Na. Mwandishi Wetu – Kibiti.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) hivi karibuni imefanya mafunzo ya Walimu Kazini kwa kipindi cha siku kumi kwa Walimu 280 wa Shule za Sekondari zilizopo katika Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani.

Akifungua mafunzo hayo Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Meja Edward Gowele, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa Walimu kazini kwani yatasaidia kuleta mabadiliko ya matokeo ambayo si mazuri katika wilaya hiyo.

"Walimu nawaomba sana mshiriki kikamilifu na kuzingatia yote katika mafunzo haya muhimu ambapo naamini mkimaliza mtaweza kuwasadia Wanafunzi shuleni kujifunza na kufanya vizuri katika mitihani yao ili kuifanya elimu ya Taifa letu kuwa na tija ya jumla katika Uchumi na Maendeleo ya nchi." Alisema Meja Gowele

Pia Meja Gowele aliishukuru TET kwa kukubali kutoa mafunzo hayo katika Wilaya ya Kibiti Mkoani Pwani kwani mafunzo hayo yanaonesha namna ambavyo Taasisi inatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau muhimu mbalimbali hapa nchini.



*Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Meja Edward Gowele*

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Ndg. Mohamed Mavura, alisema kuwa kutokana na hali mbaya ya kitaaluma wilayani hapo, uongozi unafanya juhudi za makusudi katika kuinua kiwango cha elimu katika wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Walimu wote wanapata mafunzo kazini ili kuleta mabadiliko ya kielimu.

Vilevile, Mkurugenzi wa Mafunzo ya Mitaala kutoka TET, Dkt. Fika Mwakabungu, alisema TET itaendelea kuandaa Walimu wote nchini kwa kuwapa mafunzo hayo na kuushukuru Uongozi wa Wilaya ya Kibiti kwa kushirikiana na TET katika kuandaa mafunzo hayo muhimu kwa Walimu.

Mafunzo yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Kibiti yalilenga kuwawezesha Walimu wa masomo yote kutekeleza mtaala wa umahiri kwa kuwapa mbinu mbalimbali za uwezeshaji ili kuinua kiwango cha elimu katika wilaya hiyo ambapo yatafanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ikihusisha Walimu wa masomo ya Sanaa na Lugha, na awamu ya pili ikihusisha Walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo na Biashara.

**OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)**

# PONGEZI

Tume, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tunakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu (Afya), Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

## Tunakuahidi Ushirikiano

**#Kazi Iendelee**

Dkt. Charles W. Mahera



www.tsc.go.tz    secretary@tsc.go.tz    Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

# VITABU 16 VYAPIGWA MARUFUKU KUTUMIKA SHULENI NA TAASISI ZA ELIMU

- *Yasisitizwa Mila na Desturi za Taifa kufuatwa katika kufundisha na kulea watoto;*
- *Wazazi wahimizwa kukagua mifuko ya shule ya watoto kuhakikisha vitabu hivyo havitumiki nyumbani;*
- *Ukaguzi na ufuatiliaji mashuleni kuwa endelevu;*
- *Shule itakayobainika kuendelea kuwa navyo kuchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kufutiwa uasajili; na*
- *Wajibu wa Shule kuendana na taratibu katika kuwaandaa watoto wakumbushwa.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepiga marufuku matumizi ya vitabu 16 vinavyokwenda kinyume na maadili kwenye Shule na Taasisi zote za Elimu hapa nchini.

Vitabu hivyo vimepigwa marufuku na Mhe. Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 59 cha Sheria ya Elimu Sura ya 353.

Akizungumza na Waandishi wa Habari Jijini Dodoma, Prof. Mkenda alisema kama Taifa tuna Mila na Desturi za kufuata na katika kufundisha na kulea watoto na kwamba Shule zina wajibu wa kuendana na taratibu hizo katika kuwaandaa watoto.

"Nahimiza Wazazi mkague mifuko ya shule ya wanafunzi kuhakikisha vitabu hivi havitumiki nyumbani kwani ukaguzi na ufuatiliaji huu ni endelevu ili kubaini kama vitabu kama hivi vipo katika shule tuweze kichukua hatua," alisema Prof. Mkenda

Alivitaja vitabu hivyo kuwa ni pamoja na Diary of a Wimpy Kid, Diary of a Wimpy Kid - Rodrick Rules, Diary of Wimpy Kid - The Last Straw, Diary of Wimpy Kid - Dog Days, Diary of a Wimpy Kid - The Ugly Truth, Diary of a Wimpy Kid - Cabin Fever, Diary of a Wimpy Kid - The Third Wheel na Diary of a Wimpy Kid - Hard Luck.

Vingine ni Diary of a Wimpy Kid - The Long Haul, Diary of a Wimpy Kid - Old School, Diary of a Wimpy Kid - Double Down, Diary of a Wimpy Kid - The Gateway, Diary of a Wimpy Kid - Diper Overlode, Is for TANSGENDER (You know best who you are!), Is for LGBTQIA (Find the words that make you you) na Sex Education a Guide to Life.

Aidha, Waziri Prof. Mkenda alitoa rai kwa Watanzania wote kupiga namba 0262-160270 ya mezani na 0737-962965 ya mkononi ili kutoa taarifa ya uwepo wa vitabu hivyo shuleni na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa shule yoyote itakayokutwa na vitabu hivyo ikiwemo kufutiwa usajili.

# WALIMU NA WASIMAMIZI WA ELIMU KUWEZESHWA KUBAINISHA CHANGAMOTO NA FURSA KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA STADI ZA KKK

**Na. Mwandishi Wetu – Rukwa.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kupitia Programu ya SHULE BORA (SB) inaendelea kuwezesha Walimu na Wasimamizi wa Elimu katika kubainisha changamoto na fursa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa madarasa ya Awali, la Kwanza na la Pili ili kuepusha watoto kumaliza darasa la saba bila umahiri.

Akifungua Mafunzo ya Usimamizi wa Ufundishaji wa KKK katika Shule za Msingi kwa Maafisa Elimu Mkoa (REOs) na Wilaya (DEOs), Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa, Ndg. Rashid Mchatta kupitia hotuba yake iliyosomwa na Afisa Elimu Mkoa wa Rukwa, Ndg. Samson Hango hivi karibuni alisema tatizo la watoto kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu bado ni kubwa hapa nchini.

"Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Desemba, 2022 zaidi ya Wanafunzi 25,000 kuanzia darasa la kwanza hadi la saba hawamudu stadi za KKK kwa mkoa mzima wa Rukwa. Hali hii ni hatari kwa maendeleo ya Mkoa na Taifa kwa ujumla wake." Alisema Mchatta

Kupitia mafunzo hayo ya siku tano Walimu na Maafisa Elimu toka Halmashauri nne za Sumbawanga Manispaa, Sumbawanga Vijijini, Nkasi na Kalambo watajengewa uwezo na Wataalam kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Ofisi ya Rais-TAMISEMI, SHULE BORA (SB) na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu namna ya kuwasaidia kupata umahiri wa ufundishaji KKK.

Kwa upande wake Mratibu Msaidizi wa Programu ya SHULE BORA (SB) kutoka TET Ndg. Mwesiga Kabigumila alisema, tatizo la wanafunzi kutomudu stadi za KKK linachangiwa na baadhi ya Walimu kukosa mbinu za ziada za kufundisha watoto wa darasa la Awali na la Kwanza.

Mwesiga aliongeza kuwa, Programu hiyo inakwenda kuwafikia Walimu wa Shule Arobaini (40) za Mkoa wa Rukwa wanaofundisha madarasa ya elimu ya Awali, la Kwanza na la Pili ili wapate mbinu na stadi za kwenda kusaidia wenzao shuleni.

"Katika mafunzo haya Walimu na Wasimamizi wa Ngazi ya Halmashauri watapata mbinu mbalimbali ili kuinua ari ya Watoto kupenda shule na kumudu kufundisha madarasa makubwa katika mazingira ya sasa." Alisema Mwesiga

Naye Mwezeshaji Mafunzo kutoka Chuo cha Ualimu Nachingwea Ndg. Omar Patrick alisema katika mafunzo hayo Walimu watafundishwa namna bora na rahisi ya kutayarisha zana za kufundishia Watoto wa Awali na Darasa la Kwanza ili wapende kusoma.

# TSC LUSHOTO YAENDELEA KUTOA MAFUNZO KWA WALIMU

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lushoto imeendelea kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Kazi ya ualimu. Wilaya hiyo ina jumla ya Kata 51 na walimu katika kata 15 tayari wamefikiwa na kujengewa uwezo.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Lushoto, Abihudi Hemba (wa kwanza kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Elimu wa Wilaya hiyo walipotembelea shule ya Msingi Kwemilungu.*




*Walimu wakiendelea kupata mfunzo.*

# WALIMU SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA WAPONGEZWA KWA UFAULU MZURI, 2023

- *Ni baada ya masomo yao kufaulu kwa asilimia 96 katika Mitihani ya Taifa, 2022;*
- *Hiyo imechangia katika kutekeleza majukumu muhimu ya Shirika katika kupambana na adui Ujinga, Maradhi na Umasikini;*
- *Jumla ya Walimu 15 na Mtumishi mmoka asiye mwalimu watambuliwa kwa mchango huo; na*
- *Shule ya Sekondari Kibaha, Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Shule ya Sekondari Tumbi na Shule ya Msingi Tumbi zahusika.*

**Na. Mwandishi Wetu – Kibaha.**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Ndg. Robert Shilingi, hivi karibuni katika Mkutano na Wafanyakazi aliwapongeza Watumishi Walimu na wasio walimu wa Shule za Msingi na Sekondari zilizopo chini ya Shirika la Elimu Kibaha kwa kuwezesha kupatikana kwa matokeo mazuri ya Mitihani ya Kitaifa iliyofanyika mwaka 2022.

Ndg. Shilingi alizitoa pongezi hizo kwenye mkutano huo kwa kuwazawadia Vyeti na Fedha Taslimu Watumishi hao ikiwa ni kutambua juhudi na jitihada zao ambapo kwa Walimu hao Wanafunzi walifanikisha masomo yao kufaulu kwa asilimia 96 katika Mitihani ya Taifa iliyofanyika mwaka 2022, na Watumishi wasio walimu walichangia katika mafanikio ya Kurugenzi ya Huduma za Elimu iliyopo kwenye Shirika hilo.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Ndg. Shilingi alieleza kuwa Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutekeleza majukumu yake muhimu ya kupambana na adui Ujinga, Maradhi na Umasikini kwa njia ya kutoa elimu huku akitoa pongezi kwa watumishi hao kufanikisha kufikia malengo ya Shirika.

"Kwa namna ya pekee niwapongeze Walimu na Watumishi wote wasio walimu kwa matokeo mazuri ya Mitihani ya Kitaifa katika Shule zetu zote za Msingi na Sekondari. Aidha, kwa nafasi ya pekee, nitoe pongezi kwa Uongozi wa Shule ya Sekondari Kibaha (KSS) kwa kufaulisha wanafunzi wote 91 wa Kidato cha Nne, 2022 kupata Daraja la Kwanza." Alisema Mkurugenzi Mkuu, Ndg. Robert Shilingi

Wakati huohuo, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Huduma za Elimu, Dkt. Rogers Shemwelekwa, aliwataka Watumishi kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kujenga taasisi bora na kuwezesha Shirika la Elimu Kibaha kutekeleza vyema majukumu yake kama lilivyokasimiwa.

Tuzo hizo zimetolewa kwa Walimu 15 ambao ni Filbert Kisomvu, Festo Swisbert, Deodart Joseph, Mango Kondo, Viarney Kilapilo, Hamisi Chiza, Mariam Msuya na Julius Ngasa kutoka Shule ya Sekondari Kibaha; Richard Mswahili, Rosemary Mwenda na Hajirati Abdulnul kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha; Zefania Malindila, Maulid Mputa na Eric Namadengwa kutoka Shule ya Sekondari Tumbi; na Consolata Komba kutoka Shule ya Msingi Tumbi.

Watumishi wasio walimu waliopatiwa tuzo kwa kuisaidia Kurugenzi ya Huduma za Elimu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ni Ndg. Geofrey.

# 'WAMILIKI WA SHULE ACHANENI NA VITABU VINAVYOKWENDA KINYUME NA MAADILI.' - DKT. FRANCIS MICHAEL

- *Vimekuwa na hadithi ambazo maudhui yake yanahatarisha ukuaji na malezi ya mwanafunzi;*
- *Yabainika vinapotosha mila, desturi na tamaduni za Kitanzania katika makuzi ya Watoto; na*
- *Wamiliki na waendeshaji wa shule wasisitizwa kufuata maelekezo ya Waraka Na.4 wa Mwaka 2014.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Wizara ya Elimu imewakumbusha Wamiliki wa Shule kutoingiza shuleni vitabu vyenye maudhui ambayo hayaendani na Mila, Desturi na Utamaduni wa nchi yetu.

Vitabu hivyo vimekuwa na hadithi ambazo maudhui yake yanahatarisha ukuaji na malezi ya mwanafunzi na pia kupotosha mila, desturi na tamaduni za Kitanzania katika makuzi ya Watoto na Watanzania kwa ujumla.

Akizungumza na Waandishi wa Habari Jijini Dodoma hivi karibuni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael, alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya kubaini kuwa kuna baadhi ya shule ambazo zimekuwa zikiingiza na kutumia vitabu ambavyo maudhui yake yanakinzana na maadili ya Kitanzania.

Alisema ni vizuri wamiliki na waendeshaji wa shule wakafuata Waraka Na.4 wa Mwaka 2014 uliotolewa na Wizara ambao pamoja na mambo mengine ulilenga kuhakikisha kuwa vitabu vya ziada na kiada vinavyotumika katika shule vina maudhui yanayoendana na mila, desturi na utamaduni wa nchi yetu.

"Wamiliki na waendeshaji wa Shule zote za Umma na Binafsi zilizosajiliwa hakikisheni mnafuata na kuzingatia Waraka huo pamoja na Miongozo inayosimamia elimu nchini ili kuepuka kuchukuliwa hatua za Kisheria ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili wa shule." Alisema Katibu Mkuu Michael

Alisema Wizara itaendelea kutekeleza wajibu wake wa kusimamia utoaji wa elimu na kuhakikisha njia za ufundishaji na ujifunzaji zinazingatia ubora na maslahi ya nchi.



# TSC TANGA YAWAJENGEA UWEZO WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Tanga.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga imefanya ziara katika shule za Msingi Chuda, Mabawa, Majengo na Shaban Robert kwa lengo la kuwajengea uwezo walimu juu ya mauala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu.

Ziara hizo zilizoongozwa na Kaimu Katibu Msaidizi Wilaya ya Tanga, Naima Abtwalib zilifanyika tarehe 6.2.2023 na tarehe 20.02.2023 ambapo pamoja na mambo mengine walimu walipata fursa ya kupata uelewa wa Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.

Sambamba na hilo, watumishi wa TSC katika ofisi hiyo wamejengewa uwezo juu ya masula ya VVU, magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na Rushwa mahala pa kazi.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanga, Naima Abtwalib.*




*Watumishi wa TSC Wilaya ya Tanga wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu wakati wa ziara waliyoifanya hivi karibuni kwa lengo la kuwajengea uwezo walimu juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.*




*Walimu wilayani Tanga wakiwa katika mafunzo ya kujengewa uwezo juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Tanga wakiwa katika picha ya pamoja na mkufunzi wa masula ya Magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza (mwenye tisheti nyeusi) wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika ofisi za TSC Tanga hivi karibuni.*

# TSC YASHAURIWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU ILI WASIFUKUZWE KAZI

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshauriwa kuongeza juhudi katika kuelimisha walimu juu ya haki na wajibu katika utumishi wao ili kuhakikisha hawakatishi ajira zao kutokana na kuchukuliwa hatua kwa kukiuka Miiko na Maadili ya kazi hiyo.

Ushauri huo umetolewa mwishoni mwa wiki na Afisa Elimu Msingi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Dkt. Ruth Kulang'wa wakati akifunga mafunzo ya siku tatu mjini Shinyanga ambayo yaliandaliwa na TSC kwa ufadhili wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya World Vision Tanzania.

Mafunzo hayo yaliyowakutanisha Wenyeviti wa Kamati za TSC, Watumishi wa TSC, Maafisa Elimu, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yalilenga kuandaa wakufunzi watakaotoa elimu kwa walimu katika ngazi ya shule juu ya masuala ya Ajira na Maadili katika Utumishi wa Walimu pamoja na wajibu wa jamii katika kumlinda na kumlea mtoto katika Maadili Mema.



*Afisa Elimu Msingi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Dkt. Ruth Kulang'wa akifunga mafunzo ya Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu. Mafunzo hayo yalifanyika Februari 1 - 3, 2023 mjini Shinyanga, yalilenga kuimarisha maadili na utendaji kazi wa walimu na wajibu wa jamii katika kuwalinda watoto dhidi ya ukatili.*



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Bi Fatuma Muya akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga mafunzo ya Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yaliyofanyika hivi karibuni mjini Shinyanga.*

Dkt. Kulang'wa amesema mwalimu amepewa jukumu kubwa la kumtengeneza mtoto na kumwandaa kuwa raia mwema na mwadilifu kwa manufaa ya Taifa, hivyo kutokana na wajibu huo ni vyema TSC iendelee na jukumu la kuwakumbusha walimu juu ya maadili na miiko ya kazi yao mara kwa mara na kuhakikisha wototo wanakuzwa katika maadili yanayohitajika.

"Napenda kuwapongeza TSC kwa kuwa na wazo la kuandaa andiko la kuwafikia walimu na kuwakumbusha kuhusu maadili, wajibu pamoja na haki zao. Vilevile, ninapenda kuwapongeza World Vision Tanzania kwa kuona umuhimu wa kumsaidia mwalimu kupitia TSC ili aweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo," amesema Afisa Elimu huyo.

Amefafanua kuwa pamoja na kupewa jukumu hilo kubwa, kuna walimu wapo kazini hawaelewi kabisa kama kuna wajibu unaowataka wautende kwa jamii, kwa walimu wenzao na hata kwa watoto, hivyo ni rahisi kujikuta wamefanya mambo ambayo ni kinyuime na taratibu na kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa kazi.

"Ni vizuri tuelewe kwamba Serikali haina dhamira ya kuwafukuza kazi walimu wake, sisi

# TSC YASHAURIWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU ILI WASIFUKUZWE KAZI

wadau wa elimu tunapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha tuwasaidia walimu wasikiuke masharti ya kazi. Tuwasaidie kutambua Kanuni za Utumishi wa Walimu na madhara ya kwenda kinyume na kanuni hizo ili wajiepushe na makosa," amesema Kulang'wa.

Kuhusu kumlinda mtoto dhidi ya ukatili, Afisa Elimu huyo amesema kuwa jukumu la mwalimu haliishii katika kufundisha mwanafunzi peke yake, bali ana wajibu wa kuelimisha wazazi na jamii kwa ujumla kuhusu kulinda mtoto dhidi ya ukatili anaofanyiwa ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii yatakayotokomeza kila ina ya ukatili na kufanya kila mtoto aweze kutimiza ndoto zake bila kukatishwa.

Ameleza kuwa pamoja na wajibu kuna haki za mwalimu ambazo zipo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi



*Mwakilishi kutoka Taasisi ya World Vision Tanzania, Zacharia Nyandekwa akiongea na washiriki (hawapo pichani) wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyowakutanisha Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yaliyofanyika hivi karibuni mjini Shinyanga.*

wa Umma lakini walimu hawazijui na wakati mwingine hawazipati, hivyo amewasihi Maafisa Elimu, Wathibiti Ubora wa Shule pamoja



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Bi Fatuma Muya akitoa mada wakati wa mafunzo ya Wadau wa Elimu kutoka Wilaya za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Simiyu yaliyofanyika hivi karibuni mjini Shinyanga.*

na Watendaji wa TSC kuwasaidia walimu kutambua na kupata haki zao kwa wakati badala ya kuwa kikwazo kwao.

"Katika mafunzo haya, tumefundishwa majukumu ambayo mwalimu anayo kwa mtoto, kwa jamii, kwa mwajiri na kwa walimu wenzake, lakini pia kuna haki na wajibu wa mwalimu. Hapa kwenye haki kuna vitu vingi ambavyo walimu hawavijui, na sisi ndiyo wenye wajibu kufanya walimu wazitambue na wazipate kwa wakati. Ninaomba kila mmoja aone kwamba amepewa jukumu kubwa la kufanya katika kusaidia walimu wafanye kazi katika mazingira bora ili aweze kuhudumia watoto kwa bidii, weledi, ufanisi na uzalendo," amesema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Bi Fatuma Muya amesema washiriki walijengewa uwezo katika masuala mbalimbali ikiwemo; Haki na wajibu wa mwalimu katika kazi yake, Maadili ya kazi ya ualimu, Mamlaka ya nidhamu kwa mwalimu, Utaratibu wa ajira kwa walimu, Muundo wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Nidhamu katika Utumishi wa Walimu, Uendeshaji wa Vikao vya Kamati za TSC Wilaya pamoja na Majukumu na Malengo ya Taasisi ya World Vision Tanzania.

Muya amesema washiriki hao walipata fursa ya kufanya kazi kwa vitendo katika vikundi ili kuwapima uelewa wa kile walichofundishwa kwa kuwa wanatarajiwa kwenda

# TSC YASHAURIWA KUTOA ELIMU KWA WALIMU ILI WASIFUKUZWE KAZI

kuwajengea uwezo walimu katika ngazi ya shule.

"Tunamshukuru Mungu Mafunzo yamekwenda vizuri, mada zilizowasilishwa zimeeleweka vizuri kwa washiriki, tumewapatia kazi za vikundi na hatimaye wamefanya mawasilisho ya namna watakavyotekeleleza kazi hiyo kwa walimu wetu. Tunaamini elimu hii itakuwa ni chachu ya kuleta mabadiliko kwa walimu wetu na jamii kwa ujumla ili shule zetu ziwe mahali salama kwa watoto," alisema Muya.

Naye, mwakilishi kutoka Taasisi ya World Vision Tanzania, Zacharia Nyandekwa amesema wamefandhili mafunzo hayo kwa kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu ina malengo yanayoendana na Taasisi hiyo katika kuimarisha nidhamu kwa walimu ili watoto waweze kupata haki yao ya kufundishwa na kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na ukatili.

"Niwaahidi kwamba sisi World Vision huu ni mwanzo, tunaona malengo yatu na ya TSC yanaendana, lengo kubwa ni kuwa maadili yawe mazuri shuleni na kwa jamii nzima kwa ujumla ili watoto wetu wawe salama zaidi. Tunamini kwamba World Vision Tanzania tukifanya kazi kwa ushirikiano mzuri na TSC tutaifanya Tanzania yetu iwe salama," amesema Nyandekwa.

Ameongeza kuwa World Vision Tanzania inaunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kutokomeza vitendo vyote vya udhalilishaji wa watoto pamoja na jitihada za kuwaondolea wananchi umaskini, hivyo ameahidi kutoa ushirikiano kwa ofisi za Tume hiyo zilizopo kwenye Wilaya ambazo Taasisi hiyo inafanya kazi.

"Tumeanza na mafunzo ya siku tatu hapa, lakini pia kadiri siku zinavyokwenda tutafanya mambo makubwa zaidi. Na kwa kutambua umuhimu wa mafunzo haya, tumezalisha nakala za kitini cha mwongozo wa kutolea mafunzo ambapo kwa kuanzia tutagawa vitini vinne kwa kila shule," amesema Nyandekwa.






*Washiriki wa Mafunzo wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kuandaa mpango kazi wa namna watakavyokwenda kutoa elimu kwa walimu katika ngazi ya shule mara baada ya kupata mafunzo yaliyofanyika hivi karibuni mjini Shinyanga.*



*Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Mhe. Christopher Emil Ngubiagai akitoa hotuba ya ufunguzi wa sherehe ya utoaji tuzo za Elimu katika Wilaya ya Kilwa. Sherehe hiyo ilifanyika hivi karibuni.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Kilwa, Omary Mkuwili akisoma na kukabidhi tuzo Kwa shule zilizofanya vizuri kitaaluma wilayani Kilwa.*



*Mkuu wa Wilaya ya Kilwa akicheza muziki aina ya singeli wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo za walimu wilayani Kilwa hivi karibuni.*



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Ukombozi wakitoa burudani wakati wa sherehe ya utoaji tuzo za kielimu wilayani Kilwa, hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Tunduru wakipatiwa mafunzo juu ya mapambano dhidi ya Rushwa mahala pa kazi.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Tunduru wakipatiwa mafunzo juu ya magonjwa sugu yasiyoambukiza pamoja na VVU/UKIMWI.*

# WASHIRIKI WA MAFUNZO ENDELEVU YA WALIMU KAZINI WATAKIWA KULETA MATOKEO CHANYA KWA WANAFUNZI

- *Lengo la mafunzo ni kuimarisha umahiri na weledi wa Walimu katika utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Awali na Msingi;*
- *Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK); na*
- *Mikoa sita yatajwa kushiriki mafunzo hayo*

**Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, amewataka Washiriki wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa Elimu ya Awali na Msingi (Darasa la Kwanza na la Pili) kuzingatia mafunzo hayo ili kuleta matokeo chanya kwa wanafunzi mara warudipo katika vituo vyao vya kazi baada ya mafunzo.

Mkurugenzi Mkuu huyo aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika Mkoani Morogoro.

"Tunatamani kuona gharama za mafunzo haya zinaendana na matokeo chanya kwa Wanafunzi. Washiriki mnapaswa kutumia maarifa mtakayoyapata hapa katika kusimamia vizuri suala la kutojua kusoma, kuhesabu na kuandika kwa wanafunzi. Tuzingatie na kuona umuhimu wa kuleta matokeo chanya kwa watoto." Alisema Dkt. Komba.

Mafunzo hayo Endelevu ya Walimu Kazini yaliandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kupitia Programu ya Serikali ya SHULE BORA (SB) inayofadhiliwa na UKaid yakiwa na lengo la kuimarisha umahiri na weledi wa Walimu katika utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Awali na Msingi (Darasa la Kwanza na Pili) kwa kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Aidha, Washiriki kutoka Vyuo vya Ualimu, Maafisa Elimu Taaluma, Wakuza Mitaala na Walimu Mahiri walishiriki mafunzo hayo ya siku tano (5) wakitarajiwa baada ya mafunzo hayo kwenda kuwezesha Walimu wa madarasa ya awali, kwanza na pili huku Viongozi wa Elimu Ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Shule wakitarajiwa kuwezeshwa ili kuwajengewa uelewa na uwezo wa kusimamia utekelezaji wake.

Mikoa sita (6) ya Dodoma, Mara, Pwani, Tanga, Simiyu na Rukwa ilitajwa kushiriki katika mafunzo hayo.



*Mkurugenzi Mkuu TET Dkt. Aneth Komba*

# WAZIRI MKUU AKAGUA UJENZI WA SHULE YA MSINGI YA GHOROFA INAYOJEGWA KWA MAPATO YA NDANI WILAYANI TUNDUMA

- *Ulianza kutekelezwa Desemba, 2022 na kutarajiwa kukamilika Februari, 2023;*
- *Utagharimu shilingi milioni 830 ambapo milioni 821 za Mapato ya Ndani na milioni 9 michango ya Wananchi.*

**Na. Mwandishi Wetu – Tunduma.**

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, amekagua ujenzi wa jengo la ghorofa katika Shule Mpya ya Msingi Haisoja, ujenzi unaohusisha vyumba kumi vya madarasa, ofisi nne za walimu na matundu 20 ya vyoo vya wanafunzi na matundu 4 ya vyoo vya walimu katika Halmashauri ya Mji Tunduma.

Waziri Mkuu alifanya ukaguzi huo hivi karibuni akikagua miradi inayoendelea kutekelezwa katika Kata ya Songwe na Halmashauri ya Mji Tunduma akiwa katika mwendelezo wa ziara yake mkoani Songwe.

Mradi huo wa ujenzi wa shule unatekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji na michango ya wananchi ambapo ulianza kutekelezwa tarehe 21/12/2022 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 28/02/2023.

Mradi huo hadi kukamilika unatarajiwa kugharimu jumla ya kiasi cha shilingi milioni 830, ambapo mpaka sasa umepokea kiasi cha shilingi milioni 821 za Mapato ya Ndani na shilingi milioni 9 ikiwa ni Michango ya Wananchi.





# WAZIRI MKUU AKAGUA UJENZI WA SHULE YA MSINGI YA GHOROFA INAYOJEGWA KWA MAPATO YA NDANI WILAYANI TUNDUMA

Wakati akiongea na Wananchi, Waziri Mkuu alisema, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anaendelea kuimarisha Sekta ya Elimu kwa kuhakiksha kila mtoto aliyefikisha umri wa kwenda shule anaanza masomo.

Waziri Mkuu alisema, Mheshimiwa Rais amendeleza Sera ya Elimu Bure kuanzia Darasa la Awali mpaka Kidato cha Sita na kuzuia michango kwa wazazi na walezi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mhe. David Silinde, alisema moja ya Mkakati wa Halmashauri ya Mji Tunduma ni kujenga madarasa kwa kutumia mapato ya ndani ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi darasani na kuongeza ufanisi katika ufundishaji.









# WALIMU UKEREWE WAJENGEWA UWEZO JUU YA AJIRA, MAADILI NA MAENDELEO YA UTUMISHI WAO



*Afisa Ajira na Maendeleo ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Mgreth David akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha walimu kutoka Kata ya Mukituntu kilichofanyika katika kata hiyo hivi karibuni.*

**Na Mwandishi wetu - Ukerewe**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ukerewe imefanya kikao kazi kilichowakutanisha walimu 87 kutoka katika Kata ya Mukituntu kwa lengo la kuwaelimisha juu ya Kanuni za Maadili na Utendaji kazi kwenye Utumishi wa Walimu pamoja na kuwaelimisha kuhusu majukumu ya TSC.

Kikao kazi hicho kilifanyika Februari 22, 2023 ambapo kilihusisha walimu kutoka shule za msingi za Mahande, Chabilungo, Hapembe, Kahala, Nyerere, Kahama, Kazilankanda, Kigara, Lutare na Mandela pamoja na shule moja ya Sekondari ya Mukituntu.

Katika kikao hicho Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilayani hapo, Mwl. Stephen Kushoka alisema kuwa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ni nyenzo muhimu sana ambazo Mwalimu anatakiwa kuziishi wakati wote wa Utumishi wake.

"Mwalimu anapofundisha Wanafunzi kwa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Walimu, ana uhakika wa ulinzi wa ajira yake kwa kuwa hawezi kukumbana na misukosuko ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukiuka miiko na maadili ya utumishi wake. Lakini pia mwalimu mwenye maadili mema ni kielelezo kinachomtambulisha yeye kwa wanafunzi wake na kwa watu wote au jamii inayomzunguka.

Naye Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Magreth David aliwaeleza walimu hao kuwa TSC inaandaa na kutoa nyaraka za kiutumishi kwa Walimu wa Shule za Serikali za Msingi na Sekondari Tanzania Bara na nyaraka hizo ni barua za Ajira zenye namba za usajili, kuthibitishwa kazini, kpandishwa vyeo, kupandishwa vyeo na vibali vya kustaafu hivyo kila Mwalimu anatakiwa awe na jalada nyumbani kwake kwa ajili ya kutunza taarifa zake za kiutumishi ili kuepusha usumbufu pale nyaraka hizo zinapohitajika.



*Picha ya pamoja kati ya Watumishi wa TSC wa Wilaya ya Ukerewe na walimu wa kutoka katika shule za Kata ya Mukituntu wakati wa kikao kazi kilichofanyika hivi karibuni.*




**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania